**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA PILI

## KIKAO CHA TATU

**28 JANUARI, 2016**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA PILI

## KIKAO CHA TATU – TAREHE 28 JANUARI, 2016

## I. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

## II. MASWALI YA KAWAIDA:

### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**30. MHESHIMIWA DAVID ERNEST SILINDE (MOMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Wilaya ya Momba ni moja kati ya Wilaya mpya zilizoanzishwa hivi karibuni ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi:-

Je, kwa nini Serikali imekuwa ikisuasua kutoa fedha ili ziweze kujenga ofisi na nyumba za watumishi katika makao makuu ya Wilaya ya Momba eneo la Chitete.

## OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):

### 31. MHESHIMIWA ALLY SALEH ALLY (MALINDI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira):- Hivi karibuni ulifanyika mkutano wa Dunia wa mabadiliko ya Hali ya Hewa na Mazingira (COP21) ambapo Katibu Mkuu wa UN alisema Mkataba ulioafikiwa ni "*Momental triumph for people and our planet aimed at ending poverty, strengthening peace and ensuring life of dignity and opportunity to all*":-

(a) Je, Serikali ya Tanzania ilishiriki vipi katika Mkutano huo;

(b) Je, Serikali itatekelezaje Maazimio ya Mkutano huo kisera, kisheria na kiutendaji;

(c) Je, Serikali ina mikakati gani ya kupambana na umasikini, kuimarisha amani, heshima na fursa sawa kwa kila mtu.

## WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

### 32. MHESHIMIWA NEEMA WILLIAM MGAYA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Kumekuwa na tatizo kubwa la upatikanaji wa maji katika mji wa Makambako:-

Je, Serikali imejipangaje kutatua tatizo hilo

## WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

### 33. MHESHIMIWA HAJI KHATIB KAI (MICHEWENI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:- Tanzania ni mwenyeji mkubwa kati ya nchi zilizounda Umoja wa Afrika Mashariki hivyo basi hupelekea au hupaswa watanzania kufaidika na soko la Afrika Mashariki:-

(a) Je, Serikali ya Tanzania inawashauri nini Wananchi wake wanapoenda kibiashara kwenye nchi zinazounda umoja huo;

(b) Je, pindi wanapopata matatizo au vikwazo katika nchi husika ni wapi watapeleka malalamiko.

## WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

### 34. MHESHIMIWA FREDY ATUPELE MWAKIBETE (BUSOKELO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Kwa muda mrefu Wananchi wa Busokelo wamekuwa wakikumbana na adha kubwa ya ubovu wa barabara ya Katumba – Mbambo – Tukuyu yenye urefu wa km 82 inayoanzia Katumba (RDC) kupitia Mpombo,

Kandete, Isange, Lwangwa, Mbwambo (BDC) hadi Tukuyu (RDC); na barabara hii imekuwa kwenye mpango wa kujengwa kwa kiwango cha lami kwa muda mrefu na mkandarasi yuko eneo la ujenzi wa kipande cha km 10:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha barabara hiyo kwa kujenga sehemu iliyobaki yenye km 72.

**35. MHESHIMIWA RICHARD MGANGA NDASSA (SUMVE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

Je, ni lini barabara ya Magu – Bukwimba – Ngudu – Hungumalwa itajengwa kwa kiwango cha lami.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

**36. MHESHIMIWA CECILIA DANIEL PARESSO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Katika Bunge la Kumi, aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii aliunda kamati ndogo ya kushughulikia mgogoro uliopo kati ya Wananchi wa Kata ya Buger na Hifadhi ya Taifa ya Manyara:-

(a) Je, ni nini matokeo ya Kamati ndogo iliyoundwa;

(b) Je, ni lini Wananchi watapewa taarifa ya Kamati ndogo iliyokuwa inashughulikia mgogoro huo.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**37. MHESHIMIWA FAIDA MOHAMMED BAKAR (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

Je, ni lini Benki ya Wanawake itaanza kutoa huduma zake Zanzibar.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:**

**38. MHESHIMIWA SELEMANI JUMANNE ZEDI (BUKENE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:-

Je, Serikali kupitia REA inachukua hatua gani kwa Mkandarasi CHICCO ambaye ameshindwa kukamilisha utekelezaji wa mradi wa kupeleka umeme vijijini awamu ya Pili (REA 2) katika vijiji vya Mwangoye, Mbutu na Mambali.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

**39. MHESHIMIWA CATHERINE VALENTINE MAGIGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:-

Je, ni lini Serikali itafungua rasmi kiwanda cha kutengeneza matairi cha “General Tyre” ambacho kilikuwa ni Mkombozi mkubwa kwa uchumi wa Taifa na Ajira kwa Wananchi wa Arusha.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI MKUU:**

Hoja ya kujadili Hotuba ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa wakati wa ufunguzi wa Bunge la Kumi na Moja, tarehe 20 Novemba, 2015.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA** — **DKT. T. D. KASHILILAH**
**28 JANUARI, 2015** — **KATIBU WA BUNGE**